**twiga cement**

**HEIDELBERG**CEMENT Group

# TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

# TAARIFA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka 2021 wa Wanahisa utafanyika kwa njia ya mtandao. TPC PLC inajali sana usalama kuliko mambo megine yote. Uamuzi wa kuufanya huu mkutano kwa njia ya mtandao ulifanyika ili kupunguza mikusanyiko ya watu na kulinda afya pamoja na usalama wa wanahisa wetu, wafanyikazi wetu, wakurugenzi wetu na washikadau wengine.

**Tarehe na Muda: Jumanne, tarehe 25 Mei, 2021, saa nne asubuhi**
**Uendeshaji Mkutano: Kwa njia ya mtandao, wenyeji wakiwa Chorus Call Africa**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu asome taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 28 uliofanyika tarehe 28 Mei 2020.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2020.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2020.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2021.
6. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 3 Mei, 2021**

**Brian Kangetta**
**Katibu wa Kampuni**

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**

2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwa CAD Securities Limited (kupitia anwani ya Barua Pepe: **judith@cadsecurities.com** au **neemak@cadsecurities.com** au utume picha ya fomu iliyojazwa kupitia Whatsapp [namba: **+255 777 787 845)** angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.

3. Wanahisa wanaombwa kuwasiliana na CAD Securities Limited kupitia barua pepe tajwa au namba ya Whatsapp tajwa, ili kupata maelekezo zaidi kuhusu jinsi ya kushiriki kwenye Mkutano Mkuu.

4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye tovuti ya kampuni **(https://www.twigacement.com).**